

## UTANGULIZI

Mradi wa Ujenzi wa ukuta na upandaji wa miti ya mikoko kando ya Mto Pangani, ulianzishwa kwa lengo la kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabia Nchi. Ofisi ya Makamu wa Rais kitengo cha Mazingira ambao ndio wanatekeleza mradi huu kwa ushirikiano na Wilaya ya Pangani. Wilaya yetu ni miongoni mwa Wilaya zilizo athirika na mabadiliko ya tabia nchi. Katika kukabiliana na hali hiyo, juhudi za makusudi zilifanywa na kufanikiwa kupata msaada kupitia ofisi ya Makamu wa Rais chini ya *mfuko wa kusaidia nchi zilizochini kimaendeleo* (LCDF), Wilaya zingine zinazotekeleza mradi kama huu ni Bagamoyo, Rufiji/Mafia na Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar. Kwa Wilaya ya Pangani mradi huu una sehemu kuu mbili ambazo ni *ujenzi wa ukuta wa mto Pangani na upandaji wa miti aina ya mikoko katika kingo za mto*

## ATHARI ZILIZOJITOKEZA

Maamuzi ya kutekeleza mradi huu ni kutokana na hali halisi iliyotakana na athari za mabadiliko ya tabia nchi athari ambazo zinaendelea kuongezeka siku hadi siku. Mji wa Pangani upo wastani wa mita moja chini ya usawa wa Bahari, hali inayopelekea kuathirika zaidi na majanga ya athari za mabadiliko ya tabia nchi. Ukuta ambao unasaidia sasa umejengwa wakati wa Ukoloni kwa kutumia nguvu kazi ya watumwa. Sehemu za kwanza za ukuta pande zote mbili zilijengwa na *Waarabu kabla ya mwaka 1891* na kuendelezwa na *Wajerumani kuanzia mwaka 1892* hadi walipotawala *Waingereza mwaka 1920*. Katika kipindi chote hiki kulikuwa na ukarabati na nyongeza za maeneo ya ukuta huo hadi *baada ya uhuru wa Tanganyika 1961*. Hali ya upanuzi na ukarabati vilienda sambamba na ongezeko la nguvu ya Bahari kwa maeneo yote ya Bweni na Pangani Mjini. Hali kadhalika kwa kufuata historia hiyo ni dhahiri kwamba katika *kipindi cha kuanzia miaka ya 2010* ukuta unahitaji kupanuliwa kuanzia mwisho wa eneo la mradi kupitia PANGADECOS hadi Muhembo

Miongoni mwa visababishi vya athari hizo ni kama ifuatavyo:-

- Kuongezeka kwa kina cha Bahari kulikopelekea maji kufika kwenye baadhi ya makazi ya watu na kubomoa baadhi ya barabara, hali hii ilisababishwa na kuongezeka kwa joto kulikopelekea kuyeyuka kwa barafu katika ncha ya Kaskazimi mwa Dunia miongoni mwa sababu nyingine nyingi
- Sehemu kubwa ya ardhi kuwa wazi na udongo kupelekwa baharini wakati wa mvua kutoka maeneo ya juu kulikotokana na shughuli za kibinadamu kama vile kilimo kisichozingatia taratibu, ongezeko la mifugo, ukataji miti ovyo n.k
- Nguvu kubwa ya mawimbi inayosababishwa na kuharibiwa kwa matumbawe na uoto wa misitu ya mikoko

## **1. HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

### **Kabla ya mradi huu kuanza Wilaya ilifanya mambo mengi kama yafuatayo:-**

- Kutoa elimu ya ufahamu kwa jamii juu ya athari hizo kupitia vikao mbalimbali, mikutano, mabango, sanaa na ngoma na pia kupitia miradi mbalimbali pamoja na kutumia redio Pangani FM ambayo hufikia wananchi walio wengi hapa Pangani
- Usimamizi wa sheria Kuu na ndogo katika kutumia rasilimali za Pwani kupitia dhana ya ushirikishwaji jamii
- Kupanda mikoko katika maeneo mbalimbali kando ya mto Pangani
- Kushirikisha jamii katika kusimamia rasilimali za Pwani pamoja na kuwepo kwa Mikataba ya Makubaliano (MoU)

### **Wakati wa utekelezaji wa mradi huu pia Wilaya ilifanya mambo yafuatayo:-**

- Kushirikiana na ofisi ya Makamu wa Rais kitengo cha Mazingira kwa pamoja wanatekeleza mradi huu ambao upo kwenye hatua za awali za utekelezaji kupitia ufadhili wa UNDP.
- Hadi sasa tulishapokea Tshs 18,862,400/= kwa mwaka 2015 ambazo zilipokelewa Mwezi Marchi, 2015 na zimetumika kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi, maandalizi ya Asasi na BMU, usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za mradi kwa vijiji vya Bweni, Pangani Magharibi na Pangani Mashariki
- Mwaka 2016 mwezi Juni tulipokea jumla ya Tshs 62,145,205.84 zikiwa ni Tshs 19,170,471.84 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za mradi ambapo hadi sasa hivi wastani wa Tshs 6,225,930.00 zimetumika hadi sasa. Pia zilipoklewa jumla ya Tshs 42,974,734.00 kwa ajili ya elimu ya ufahamu, mafunzo na upandaji mikoko. Utekelezaji wa shughuli kwa fedha hizi za jamii utanza mara ya ujenzi wa ukuta kuanza na kamati za BMU zitakapo kamilisha uchaguzi ambao unaendeshwa na Ofisi ya Uvuvi

Mradi pia utapanua shughuli zake hadi vijiji vya jirani na vile vya awali ambavyo ni Mkwajuni, Msaraza na Mwembeni

Shughuli kuu zilizofanyika hadi sasa hivi ni hizi zifuatazo:-

- Kupata taarifa za awali (*Baseline study*) juu ya ukuta, uchumi wa kijamii
- Kutoa zabuni kwa wataalamu wa Kimataifa kwa ajili ya ujenzi wa ukuta
- Kupata taarifa mpya na kufanya mapitio ya taarifa za awali
- Kuhudhuria vikao vya nje ya mkoa
- Kutoa mafunzo kwa maafisa 65 kwa ngazi ya utekelezaji (Technical Officers) katika mabadiliko ya tabia nchi pamoja
- Kufanya ufuatiliaji wa hali ya ukuta na kujifunza kwa majirani mbinu za hifadhi ya bahari
- Kutoa mafunzo kwa kamati za kusimamia maeneo ya Pwani (Beach Management Unit) kwa kuwafundisha elimu ya mikoko na utnzaji wake hadi kuweza kurudishia uoto wa mikoko kwa kutumia nguvu zao

- Tathimini ya maeneo yatakayopandwa mikoko kando ya mto
- Kujenga uwezo kwa wananchi, Serikali za Vijiji kuzunguka eneo la mradi na kuwezesha kupewa kazi ya kupanda mikoko
- Kusimamia ukamilishaji wa taratibu za Kimazingira, kama vile tathimini ya awali kwa athari za Mazingira na Jamii (Scooping on EIA), Uafiti wa hali ya umbile la ndani na nje ya ardhi (Geodetic and Topographic survey)

## 2. UTEKELEZAJI

Mradi huu utatekelezwa kupitia miradi mikuu miwili

Yafuatayo ni maelezo ya kila mradi:-

1. **Ujenzi wa ukuta wa mto Pangani Meta 1810 za urefu** (Pangani Mjini meta 1,145 na Bweni meta 665), chini ya Mradi wa namna ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi kwenye Miundombinu na Makazi (*Addressing Climate Change Impacts on key infrastructure and settlements*). Mkandarasi ambaye ni UNOPS ameshasaini mkataba. Mradi huu unategemewa kuanza kazi zake muda wowote kuanzia sasa, taratibu za manunuzi zimkamilika katika ngazi ya Kimataifa, tangazo la kuwapata *wakandarasi wenza* limetolewa tarehe 11/03/2016 kupitia magazeti ya Mwananchi, The Guardian na zabuni hiyo ilifungwa tarehe 21/03/2016 na ukaguzi ulishafanyika mara mbili mwezi Mei 26, na Agosti 11/2016. Hadi sasa taarifa za ujenzi hazijapatikana rasmi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais

2. **Upandaji wa miti ya mikoko Hekta 10.** Mradi wa Kukabiliana na athari za tabia nchi kutumia vipaumbele kama kwa kupanda mikoko katika ukanda wa Pwani kwa kurudishia uasilia wa mahali (*Priority adaptation interventions for resilient Integrated Coastal Zone Management*). Katika mradi huu yafuatayo yatazingatiwa:-

BMU za Bweni, Pangani Magharibi na Mashariki zimepewa zabuni/jukumu la kurudishia uoto huo kupitia kwa Mtaalamu mshauri wa Mikoko ngazi ya Taifa. Katika hili jamii itashiriishwa katika utunzaji wa fukwe. Pia vitalu vya miche ya mikoko vitaanzishwa kwa kushirikisha ASASI za kiraia

Mtaalamu mshauri wa Mradi wa kupanda mikoko alishauri kuongeza vijiji vya Mkwajuni, Msaraza na Mwembeni ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na uhimilivu na uendelezaji wa jambo hili kwa kuwa vijiji hivyo vipo kwenye ikolojia moja ya bonde la Mto Pangani kwa hali hii ukubwa wa eneo litakalopandwa mikoko utaongezeka kama mara mbili hivi

## **HALI ILIVYO HADI SASA**

### **2.1. HALI YA UKUTA**

Hali ya ukuta hadi sasa bado ukuta unaendelea kuharibika japo sio kwa kasi kubwa kama ilivyokuwa mwanzo, kwani jitihada za Halmashauri za kukarabati sehemu zilizoathirika zilifanyika

- Juhudi za kupanda mikoko zinaendelea kwa kuwashirikisha jamii
- Iliazimiwa kuwa lazima ukuta unaojengwa ulenge kudumu/kuishi kwa muda wa miaka mia moja badala ya miaka hamsini
- Wakati mradi huu utakapotekelezwa Wilaya zinazotekeleza zitasaidiwa kuendesha zoezi la uelewa wa wananchi

### **5.2 HALI YA ENEO LA PANGADECOS**

- Hali ya eneo hili sio ya kuridhisha kwani kuna kasi kubwa ya mmomonyoko wa kingo za bahari ambao unahitaji kudhibitiwa mapema. Wataalamu wa Wilaya kwa kushirikiana na wananchi hasa BMU tupo kwenye mchakato wa kutathimini athari hizo pamoja na kuandaa taarifa ya uharibifu huo ili kuwasiliana na mamlaka za juu kupata ufumbuzi wa tatizo hili. Ni imani yetu kuwa kupitia taarifa hii na maombi ya viongozi mbalimbali kunu kama chombo cha kutoa maamuzi tutapata ufumbuzi wa jambo hili la PANGADECOS